

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM


**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com




## MATANGAZO: DOMINIKA 29 YA MWAKA C - 19.10.2025

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA 19.10.2025 | **DOMINIKA YA 29 YA MWAKA C WA KANISA**<br>DOMINIKA YA MISIONI<br>Ujumbe wa Baba Mtakatifu: Wamisionari wa Matumaini kwa Watu Wote.<br>Mchango wa pili kwa ajili ya Uenezaji wa Injili (Misioni). |
| 2. | JUMATANO 22.10.2025 | Kumbukumbu ya Mt. Yohane Paulo II, Papa |
| 3. | JUMAMOSI 25.10.2025 | Kutakuwa na Misa ya kuhitimisha matembezi ya Sanamu ya Bikira Maria katika **Kanda D na E** saa 1:00 asubuhi na kukabidhi Sanamu kwa **Kanda F na G**.<br>Jumuiya zinatakiwa kuhimiza na kufuatilia bahasha za Kapu la Mama na kuzirejesha katika Misa za kuhitimsha matembezi ya sanamu. |
| 4. | JUMAMOSI 25.10.2025 | Kutakuwa na Misa kwa heshima ya wasimamizi wa Jumuiya za Mt. Theresa wa Avila na Mt. Yohane Paulo II saa 10:00 jioni. |
| 5. | DOMINIKA 26.10.2025 | **DOMINIKA YA 30 YA MWAKA C**<br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Padre Pio<br>Watangaza Neno: Angela Ramadhani na Hans Kahumba<br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Yohane Krisostom<br>Watangaza Neno: Zawadi Jackson na Baptis Komba<br>**Misa ya 3: Saa 5:00 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Padre Pio na Mt. Yohane Krisostom<br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya Utume wa Familia. |
| 6. | MAFUNDISHO YA KOMUNYO NA KIPAIMARA | Mafundisho Kipaimara na Komunyo ya Kwanza yameanza rasmi wiki iliyopita na leo kutakuwa na kikao cha wazazi na walezi wa mara baada ya Misa ya kwanza. Mafundisho yataendelea Jumamosi ijayo saa 3:00 asubuhi. |
| 7. | RATIBA YA MAVUNO PAROKIA 2025 | Tulizindua Mavuno Parokia Dominika ya 05.10/2025, viongozi wa Jumuiya wanatakiwa kufuatilia familia ambazo bado kuahidi na walioahidi kuanza kukamilisha na mwisho ni siku ya kilele 02.11.2025 tutakapopokea na kufanya mnada wa mavuno ya vitu.<br>Kilele cha Mavuno Jimbo ni Jumamosi 22.11.2025 |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | VITI VYA PAROKIA | Parokia ipo mbioni kununua viti vipya. Hivyo viti vinavyotumika sasa ukumbini vinauzwa kwa Jumuiya zinazohitaji kwa bei ya kati ya sh. 5,000 na 10,000/=. Wanaohitaji wawasilishe barua au kulipa kabla ya Dominika ijayo. |
| 9. | UCHAGUZI WA VIONGOZI WA VYAMA KANDA | Jumamosi ijayo tutasali katika Kanda na kufanya uchaguzi wa Vyama vya Wazee na Wastaafu na VIWAWA Kanda. Kanda ambazo hazikufanya uchaguzi wa UWAKA na WAWATA wiki iliyopita zihakikishe zinakamilisha chaguzi za vyama hivyo vinne wiki ijayo. |
| 10. | MATANGAZO YA KWAYA | Kwaya ya Mt. Yohane Paulo II wiki ijayo watasherehekea sikukuu ya Msimamizi wao, na watakuwa na wageni wa Kwaya ya Mt. Antoni wa Padua Kwembe watakaoimba nao Misa ya kwanza na ya pili na baadaye tafrija ya kubadilishana uzoefu.<br><br>Kwaya ya Vijana ya Kung'ara kwa Yesu Kristo watakuwa na ziara ya kuinjilisha katika Kituo cha Malezi Child in the Sun Dominika ijayo. |
| 11. | MAREJESHO YA VITABU | Jumuiya zinakumbushwa kufanya malipo ya vitabu vya Liturujia ya Sikukuu ya sikukuu ya Parokia tarehe 10.08.2025. |
| 12. | KIKAO CHA WANAUME WOTE | Kutakuwa na kikao kifupi cha wanaume wote Dominika ijayo mara baada ya Misa ya kwanza. |
| 13. | WARSHA YA WAAMINI WOTE JIMBO | Warsha ya waamini wote wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam itafanyika Jumamosi 29.11.2025 katika viwanja vya Parokia ya Kristo Mfalme Tabata kuanzia saa 2:00 asubuhi. Kutakuwa na Mada mbili,<br>1. Uchaguzi/Uongozi katika Kanisa 2. Mwaka wa Jubilei Kuu<br>Kutakuwa pia na vyeti kwa wenye Jubilei za miaka 25, 50 na 75.<br>Ada ya ushiriki ni 5,000/=.<br>***Kila Jumuiya inatakiwa kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya uandikishaji washiriki wa Warsha kwani inatakiwa Jimboni.*** |
| 14. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini Letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kauli Mbiu ya Mwaka wa Jubilei Kuu: "Jubilei 2025 – Mahujaji wa Matumaini."***

**MATEMBEZI YA SANAMU YA BIKIRA MARIA KATIKA MWEZI WA ROZARI NA KAMPENI YA KAPU LA MAMA MARIA 2025**

| WIKI | TAREHE | KANDA HUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | 28/09 - 04/10 | A |
| 2 | 04/10 – 11/10 | B |
| 3 | 11/10 – 18/10 | C |
| 4 | 18/10 – 25/10 | D & E |
| 5 | 25/10 – 01/11 | F & G |
| 6 | 01/11 – 08/11 | H |
| 7 | 08/11 – 15/11 | I |
| 8 | 15/11 – 22/11 | J |
| 9 | 22/11 – 29/11 | K |

**MATANGAZO NDOA KWA MARA YA KWANZA**

1. Frank Samwel Mruma BIN Samwel Simon Mruma na Maria Rajabu Mchomvu wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

Anatarajia kufunga ndoa na:

Lightness Anold Mariki BINTI Anold Yohane Mariki na Kristina Makyao wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

2. Nobert Alfons Matage BIN Alfons Matage na Theodosia Mbanga wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

Anatarajia kufunga ndoa na:

Anna Raphael Mngazija BINTI Raphael Mngazija na Aisha (Suzana) Ramadhani wa Parokia ya Mbezi Mshikamano

**MASOMO DOMINIKA YA 30 YA MWAKA C – 26.10.2025**

| | |
|---|---|
| SOMO I | YbS 35:12-14, 16-19 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 34: 1-2, 16-18, 22 |
| SOMO II | 2Tim 4:6-8, 16-18 |
| SHANGILIO | Yn 8:12 |
| INJILI | Lk 18:9-14 |